

KUENDELEA KUSTAHIKI KWA MEDICAID



Mnamo 2020, Serikali ya Shirikisho iliweka sheria maalum zilizokomesha kusitisha huduma ya Medicaid kwa sababu ya Janga la COVID-19. Sheria hizi zimebadilika hivi karibuni. Jimbo la Vermont sasa litaanza mchakato wa kawaida wa kuendelea kustahiki kwa Medicaid mnamo mwezi wa Aprili. Utaendelea kustahiki kupata Medicaid ikiwa bado unakidhi mahitaji ya mapato, umri na makazi. Ikiwa hustahiki tena, huduma yako ya bima inaweza kusitishwa. Hili likitokea, utakuwa na nafasi ya kujiandikisha kwa aina nyingine za bima. **Ofisi ya Wakili wa Huduma za Afya iko hapa kukusaidia ikiwa una maswali au wasiwasi kuhusu mchakato wa kuendelea kustahiki kwa Medicaid.**

Kuendelea kustahiki kwa Medicaid:

Mchakato wa kuendelea kustahiki kwa Medicaid utanza tena mnamo Aprili 2023. Vermont Health Connect (VHC) itakutumia barua ya kuendelea kustahiki ikikuomba taarifa. Wanaweza kukuomba uwatumie taarifa ili wathibitishe kwamba unakidhi mahitaji ya mapato, makazi na umri ili uendelee kupata huduma za Medicaid. Huenda ukahitaji kutoa uthibitisho wa mapato yako ya sasa.

Hawatashughulikia huduma zote za Medicaid mara moja. Badala yake, watatuma barua kadhaa za kuendelea kustahiki katika kipindi cha miezi 14 ijayo. Kujibu barua hizi na kupea VHC taarifa wanazoomba ni muhimu.

Sasisha Maelezo Yako ya Mawasiliano:

Unapaswa kuhakikisha kuwa VHC ina anwani yako ya sasa ya barua ya posta, nambari ya simu, na barua pepe kwenye faili zao ili waweze kukutumia barua ya kuendelea kustahiki na masasisho mengine muhimu.

Wapigie simu namba ni **855-899-9600** au ingia kwenye tovuti yako kwa kutembelea **vermonthealthconnect.gov** ili uthibitishe kuwa taarifa hii ni ya kisasa.

Notisi ya Kusitisha Huduma:

Utaendelea kustahiki kupata Medicaid ikiwa bado unakidhi mahitaji ya mapato, umri na makazi. Lakini Iwapo hustahiki tena kwa huduma ya Medicaid, VHC lazima ikutumie notisi ya kusitisha huduma kabla ya manufaa yako kuisha. Ni lazima wakupe notisi kabla ya tarehe ya kusitisha huduma. Huduma ya Medicaid haitasitishwa hadi siku ya mwisho ya mwezi uliopangwa.

Kipindi Maalum cha Kujiandikisha:

Iwapo hustahiki tena kwa Medicaid na huna huduma ya Medicare, unaweza kupata Kipindi Maalum cha Kujiandikisha ili ujiandikishe kwenye mpango wa bima ya afya kupitia VHC bima yako itakapoisha. Utakuwa na **siku 60** baada ya huduma yako ya Medicaid kusitishwa ili ujiandikishe kwenye mpango wa bima kupitia VHC.

Ikiwa mwajiri wako atatoa bima, unaweza kujiandikisha kwenye mpango huo wa bima wakati huduma yako ya Medicaid inasitishwa. Lakini ni muhimu kuchukua hatua haraka. Kipindi Maalum cha Kujiandikisha kwenye mpango wa bima ya mwajiri kinaweza kupunguzwa hadi siku 30.

Medicare:

Pigia simu Ofisi ya Wakili wa Huduma za Afya kwa ushauri wa kibinafsi ikiwa una huduma ya Medicare na una maswali kuhusu Medicaid na machaguo yako ya bima.

Tupigie simu ukiwa na Maswali:

Ofisi ya Wakili wa Huduma za Afya ni rasilimali ya bure na ya siri kwa wakaazi wa Vermont walio na maswali kuhusu bima ya afya au upatikanaji wa huduma. Tupigie simu ikiwa una maswali kuhusu jinsi mchakato wa kuendelea kustahiki kwa Medicaid au suala lingine lolote linalohusiana na afya. Unaweza kupigia simu Huduma yetu ya Usaidizi namba ni **1-800-917-7787**. Unaweza pia kupata taarifa zaidi kwenye tovuti yetu au kuwasilisha ombi la usaidizi mtandaoni kwa vtlawhelp.org/health.